


HALMASHAURI YA WILAYA YA GAIRO



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo anayofuraha kutangaza nafasi za ajira **MARUDIO** nafasi ya katibu muhtasi Daraja III nafasi mbili (2), Ajira hizi zinatokana na kibali cha ajira kutoka kwa katibu mkuu ofisi ya rais, menejimenti ya utumishi wa umma na utawala bora kutekeleza ikama ya bajeti kwa ajira mpya katika mwaka wa fedha 2021/2022. Kibali cha Ajira chenye Kumbukumbu Na. FA.228/01/9 Cha Tarehe 13 May, 2022.

1.0 NAFASI ZINAZOTANGAZWA:

1.1 Katibu muhtasi III (Nafasi 2)

- **Kazi na Majukumu**

- i. Kuchapa barua na nyaraka mbalimbali
- ii. Kusaidia kupokea wageni na kuwa saili shida zao, na kuwaelekeza sehemu sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- iii. Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miradi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizo pangwa kutekelezwa katika ofisi anayofanyia kazi na kumtaarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- iv. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- v. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- vi. Kutekeleza kazi zote atakazokuwa amepangiwa na msimaamizi wake wa kazi.

- **Sifa za Mwombaji:**

Awe na Elimu ya kidato cha IV au V, Awe amehudhuria mafunzo ya Uhazili, Awe amefaulu somo la Hati Mkato ya Kiingereza na Kiswahili maneno 80 kwa dakika moja na Awe amehudhuria na kufaulu mafunzo ya kompyuta kutoka Chou chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata Cheti katika program za Windows, Microsoft Office, Internet, E Mail na Publisher.

- **Mshahara:**

Kwa kuzingatia ngazi ya Mishahara ya Serikali **TGS B1** kwa mwezi.

2.0 MASHARTI YA JUMLA:

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania.
2. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
3. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba za simu pia majina mawili (2) ya wadhamini yakiwa na anuani kamili.
4. Maombi yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma na vyeti vya kuhitimu mafunzo ya vyeti.

5. Maombi yaambatanishwe na picha mbili (2) passport size ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
6. Mwombaji aandike nafasi ya ajira anayoomba nyuma ya bahasha.
7. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 25 Oktoba, 2022 saa 9:00 Alasiri

3.0 NJIA YA KUTUMA MAOMBI:

Maombi yatumwe Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kwa anuani ifuatayo:

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Gairo,
S.L.P. 40,
GAIRO.

WAOMBAJI WOTE WANAKARIBISHWA

Limetolewa Na:

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA GAIRO

M. Haule
Msifwaki N Haule

KAIMU MKURUEGNI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
GAIRO